**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# MKUTANO WA SABA

# YATOKANAYO NA KIKAO CHA KUMI NA MOJA

**24 APRILI, 2017**

**MKUTANO WA SABA**

**KIKAO CHA KUMI NA MOJA TAREHE 24 APRILI, 2017**

## I. DUA:

Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi na Mwenyekiti wa Bunge Mhe. Mussa A. Zungu alisoma Dua na kukiongoza Kikao.

Makatibu mezani:

1. Ndugu Theonest Ruhilabake
2. Ndugu Charles Mloka
3. Ndugu Zainab Issa

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

(i) Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Prof. Palamagamba J. Kabudi aliwasilisha mezani Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018;

(ii) Kwa Niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Naibu Waziri Mhe. Luhanga J. Mpina aliwasilisha mezani Hobuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofis hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018;

(iii) Taarifa ya Kamati ya Katiba na Sheria kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kwa Mwaka 2016/2017 pamoja na maoni ya Kamati ya juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018;

(iv) Taarifa ya Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018;

(v) Mhe. Pauline Gekul aliwasilisha mezani Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Upinzani kuhusu Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) juu ya makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018;

(vi) Mhe. Pauline Gekul aliwasilisha mezani Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) juu ya makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

## III. MASWALI

### OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA)

Swali Na. 85: Mhe. Ruth Hiyob Mollel (kwa niaba yake Mhe. Peter S. Msigwa aliuliza swali hilo)

Nyongeza: Mhe. Peter S. Msigwa
Mhe. David E. Silinde
Mhe. Mary P. Chatanda

### OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA)

Swali Na. 86: Mhe. Omary M. Kigua

Nyongeza: Mhe. Omary M. Kigua
Mhe. Yussuf S. Hussein

### WIZARA YA KATIBA NA SHERIA

Swali Na. 87: Mhe. Mohamed A. Mohamed

Nyongeza: Mhe. Mohamed A. Mohamed
Mhe. Ally S. Ally
Mhe. Mariam S. Msabaha
Mhe. Joseph R. Selasini

Swali Na. 88: Mhe. Philipo A. Mulugo

Nyongeza: Mhe. Philipo A. Mulugo
Mhe. Susan A. Lyimo
Mhe. Mwita M. Waitara

## WIZARA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI

Swali Na. 89: Mhe. Hawa S. Mwaifunga

Nyongeza: Mhe. Hawa S. Mwaifunga

Swali Na. 90: Mhe. Dkt. Christine G. Ishengoma

Nyongeza: Mhe. Dkt. Christine G. Ishengoma

Swali Na. 91: Kwa niaba ya Mhe. Dkt. Rashidi M. Chuachua, Mhe. Nape M. Nnauye

Nyongeza: Mhe. Nape M. Nnauye

## WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Swali Na. 92: Mhe. Hassan E. Msala

Nyongeza: Mhe. Hassan E. Msala
Mhe. Musukuma J. Kasheku
Mhe. Zuberi M. Kuchauka
Mhe. Catherine V. Magige
Mhe. Frank G. Mwakajoka

## WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO

Swali Na. 93: Kwa niaba ya Mhe. Hawa M. Chakoma, Mhe. Faustine E. Ndugulile aliulliza

Nyongeza: Mhe. Faustine E. Ndugulile

Swali Na. 94: Mhe. Martha J. Umbula

Nyongeza: Mhe. Martha J. Umbula

## IV. MATANGAZO:

### WAGENI

Wageni mbalimbali walioko kwenye *Galleries* za ukumbi wa Bunge walitangazwa.

### MWONGOZO WA SPIKA

1. Mhe. Kapunda aliomba mwongozo kwamba Bunge liahirishe shughuli zake na kujadili suala la wachimbaji wadogo wa mgodi wa dhahabu Kitunda ambao waliodondokewa na machimbo hayo na kutolewa maiti takribani 5 na kwamba kinachoonekana ni kwamba Serikali haina idadi kamili ya wachimbaji waliopo maeneo hayo kwa kuwa inasema kuwa wanakadiriwa kuwa 5000 – 7000 na kwamba hata usajili na usimamizi wake si mzuri.

   Kiti kiliagiza Serikali kulifanyia kazi suala hilo kwa kushirikiana na Mbunge husika ili kupata ufumbuzi.

2. Mhe. Said A. Kubenea Kifungu 68(7) aliomba mwongozo juu ya upi ni msimamo wa Serikali katika usimamishaji na ufukuzaji wa Watumishi kati ya ule uliotolewa na Waziri wa Utumishi na Utawala Bora wakati akijibu Swali na. 87 na ule uliotolewa na Mhe. George B. Simbachawene, Waziri wa TAMISEMI.

   Kiti kilimpa nafasi Mhe. George B. Simbachawene kutoa ufafanuzi naye alifanya hivyo.

## V. HOJA ZA SERIKALI

1. Mawaziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Januari Y. Makamba alitoa hoja yake kwamba Bunge sasa likubali kupitisha makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

2. Mjumbe kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria aliwasilisha Taarifa na maoni ya Kamati hiyo kuhusu (Muungano).

3. Mhe. Mary M. Mwanjelwa kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira aliwasilisha Taarifa na maoni ya Kamati hiyo kuhusu (Mazingira).

4. Mhe. Ally S. Ally aliwasilisha Taarifa ya Kambi ya Upinzani (Muungano) ya Ofisi ya Makamu wa Rais na kupewa maelekezo na kiti ya kuondoa uk. 4, 5, 7 na mstari wa mwisho wa para ya 1 na ya 2 na maneno kisu cha ngariba katika para ya 3.

5. Mhe. Pauline P. Gekul aliwasilisha Taarifa ya Kambi Rasmi ya Upinzani (Mazingira) ya Ofisi ya Makamu wa Rais.

## VI. KUSITISHA BUNGE

Shughuli za Bunge zilisitishwa saa 7:00 mchana hadi saa 11:00 jioni.

## VII. SHUGHULI ZA BUNGE KUREJEA

Shughuli za Bunge zilirejea saa 11:00 jioni na Waheshimiwa Wabunge wafuatao walipata nafasi ya kutoa michango yao kwenye Hoja ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kwamba Bunge likubali kupitisha makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

1. Mhe. Ahmed Juma Ngwali - CUF
2. Mhe. Shamsi Vuai Nahodha - CCM
3. Mhe. Asha Abdullah Juma - CCM
4. Mhe. Stanslaus Haroon Nyongo - CCM
5. Mhe. Immaculate Sware Semesi - CHADEMA
6. Mhe. Ali Hassan Omar King - CCM
7. Mhe. Khadija Hassan Abeid - CCM
8. Mhe. Aeshi K. Hillary - CCM
9. Mhe. Waziri wa Nishati na Madini, Prof. Sospeter Mwijarubi Muhongo
10. Mwanasheria Mkuu wa Serkali, Mhe. George Mcheche Masaju
11. Mhe. Dkt. Ashatu K. Kijaji, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango
12. Mhe. Angellah Jasmine Kairuki, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora)
13. Mhe. Luhaga J. Mpina, Naibu wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira)

Mhe. Januari Y. Makamba, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) alihitimisha hoja yake kwa kujibu hoja zilizojitokeza wakati wa mjadala.

## VIII. KAMATI YA MATUMIZI

### Fungu 26 – OFISI BINAFSI YA MAKAMU WA RAIS

Waheshimiwa wafuatao walipata ufafanuzi:-

1. Mhe. Masoud A. Salim – Fungu hili liliafikiwa

### FUNGU 31 – OFISI YA MAKAMU WA RAIS

Wafuatao waliomba ufafanuzi kwenye mshahara wa Waziri:-

1. Mhe. Pauline P. Gekul
2. Mhe. Hashim Jaku
3. Mhe. Jitu V. Soni

Mhe. Jenista J. Mhagama alitoa ufafanuzi wa *concern* ya Mhe. Jitu Soni na kuomba hoja yake iende mwishoni mwa bajeti wakati wa kuhitimisha Bajeti ya Serikali na Mhe. Jitu Soni alikubali.

4. Mhe. Ahmed Juma Ngwali alitoa hoja ya kuondoa shilingi na Wabunge wafuatao walichangia:-

   (i) Mhe. Khatib Said Haji
   (ii) Mhe. Ally Saleh Ally
   (iii) Mhe. Said Kubenea
   (iv) Mhe. Sospeter Muhongo, Waziri wa Nishati na Madini alitoa ufafanuzi
   (v) Mhe. Prof. Palamagamba Kabudi, Waziri wa Katiba na Sheria alitoa ufafanuzi.
   (vi) Mhe. Luhaga J. Mpina alitoa ufafanuzi
   (vii) Mhe. Jenista J. Mhagama – ufafanuzi wa jambo lililotolewa na Mhe. Ngwali.

*Guillotine:* FUNG 31 – Matumizi ya Kawaida na Maendeleo lilipitishwa kwa *Guillotine.*

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) alitoa taarifa na Mwenyekiti wa Bunge alihoji Bunge na Bajeti ya Wizara hiyo ilipitishwa.

## IX. KUAHIRISHA BUNGE

Shughuli za Bunge ziliahirishwa saa 2:15 usiku hadi kesho tarehe 25 Apirli, 2017 saa 3:00 asubuhi.